



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
**HALMASHAURI YA JIJI ARUSHA**



Barua zote zitumwe kwa:

Simu: +255 27 2548072/2503494 (Director)

+255 27 2544330 (General)

Nukushi: +255 27 2545768

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. AB. 156/423/01

Mkurugenzi wa Jiji  
S. L. P. 3013,

20 Barabara ya Boma,  
23101 ARUSHA,

Barua Pepe: [cd@arushacc.go.tz](mailto:cd@arushacc.go.tz)

Tovuti: [www.arushacc.go.tz](http://www.arushacc.go.tz)

Tarehe: 13 Machi, 2023

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Jiji la Arusha imepokea kibali cha ajira mbadala chenye Kumb. Na. FA. 170/371/01A" /172 cha tarehe 16 Februari, 2023. Hivyo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Jiji la Arusha kutuma maombi ya kazi kwa Mkurugenzi wa Jiji ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya Tangazo hili

SN	KADA	IDADI YA NAFASI	SIFA ZINAZOTAKIWA
1	Mtendaji wa Mtaa III (TGS B1)	2	(a) Awe Raia wa Tanzania na Mwenye akili timamu (b) Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45 (c) Awe na elimu ya Kidato cha Nne au Sita na Astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo:- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali

### **Kazi na Majukumu ya Mtendaji wa Mtaa:**

- (a) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Mtaa
- (b) Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Mtaa
- (c) Kuratibu na kusimamia upangaji wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Mtaa
- (d) Katibu wa Mikutano au Kamati zote za Halmashauri ya Mtaa
- (e) Kutafsiri na kusimama Sera, sheria na taratibu
- (f) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi zote za Halmashauri ya taa
- (g) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- (h) Kiongozi wa wakuu wa Vitengo vya kitaalam katika mtaa
- (i) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka zote za mtaa.

### **MAELEZO YA JUMLA**

- a) Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vya Elimu/taaluma, cheti cha kuzaliwa na maelezo binafsi (CV.
- b) Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA.
- c) Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Jumatatu ya tarehe

**27/03/2023 saa 9:30 alasiri.**

Maombi yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi,  
Halmashauri ya Jiji la Arusha,  
S.L.P. 3013,  
ARUSHA.**

Tangazo hili limetolewa na:

Hargeney R. Chitukuro  
MKURUGENZI WA JIJI  
ARUSHA



Nakala;- - Kwenye mbao za Matangazo